# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA

**TAARIFA INATOLEWA KUWA** Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa wa Benki ya Biashara Mkombozi utafanyika tarehe **26 Julai, 2025** kuanzia saa tatu asubuhi katika Ukumbi wa Selous unaopatikana ndani ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), Posta, Dar es Salaam.

**AJENDA**

1. Kuthibitisha akidi na Kufungua Mkutano;
2. Kupitishwa kwa Ajenda ya Mkutano;
3. Kuthibitisha dondoo za Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 15 uliofanyika tarehe 27, Julai, 2024;
4. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 15 uliofanyika tarehe 27 Julai, 2024
5. Kupokea, kujadili na kuidhinisha taarifa ya Wakurugenzi ya mwaka ulioishia tarehe 31Desemba, 2024;
6. Kupokea, kujadili na kuidhinisha taarifa ya fedha ya Benki kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2024 pamoja na kupokea taarifa ya Mkaguzi wa Nje wa hesabu juu ya taarifa hiyo ya fedha;
7. Kupokea, kujadili na kuidhinisha pendekezo la Gawio kwa Mwaka 2024;
8. Kuteua Mkaguzi wa nje wa hesabu za Benki;
9. Kuteua Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi;
10. Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka ujao;
11. Mengineyo;na
12. Kufunga Mkutano.

**MAELEZO:**

1. Mwanahisa anayetaka kuhudhuria Mkutano Mkuu wa mwaka anapaswa kuja na nakala ya stakabadhi ya ununuzi wa Hisa au Cheti cha Hisa cha kumtambulisha kua ni Mwanahisa.

2. Mwanahisa mwenye stahili ya kuhudhuria mkutano huu ana haki ya kumteua mwakilishi wake wa kupiga kura kwa niaba yake kwa mujibu wa taratibu za kampuni. Fomu husika inayopaswa kujazwa na Mwanahisa kwa



CamScanner

ajili ya uteuzi huo inatakiwa kufikishwa kwa katibu wa Benki siku tatu kabla ya mkutano. Kwa taasisi, fomu inapaswa kuwa katika lakiri ya taasisi Mwanahisa. Fomu hiyo iandikwe kama ifuatavyo.

**Benki ya Biashara Mkombozi**

Mimi/Sisi……………………….......................………………..............wa…… ………….........................................................., nikiwa/tukiwa Mjumbe/Mwanahisa wa kampuni iliyotajwa hapo juu, ninamteua/tunamteua ..................................................... wa ...................................................... ........................................ kama mwakilishi wangu/wetu kupiga kura kwa niaba yangu/yetu katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa wa Benki utakaofanyika terehe 26 Julai, 2025.

Saini .......................................................

Imetolewa leo tarehe………………Mwezi…………………2025.

3. Wanahisa wote na/au wawakilishi wao watahitajika kujisajili kwanza kabla ya kuingia kwenye ukumbi siku ya mkutano.

4. Vitabu vyote vilivyo na ripoti za kifedha na taarifa nyingine muhimu za benki vitapatikana kwenye matawi ya Benki na tovuti ya Benki https://mkombozibank.co.tz/ wiki tatu kabla ya mkutano.

Kwa maelezo na taarifa zaidi, wasiliana na Ofisi ya Benki kwa anuani ifuatayo:

Benki ya Biashara Mkombozi,
Kiwanja Namba 40, Nyuma ya Kanisa la Mtakatifu Yosefu,
Mtaa wa Mansfield,
S.L.P 38448,
DAR ES SALAAM.
Namba za Simu: +255 22 2137806/7.
Namba ya bure ya maulizo: 0800 750 040
Barua Pepe: shareholders@mkombozibank.co.tz

**PAULINA KUNJUMU**
**KATIBU NA MWANASHERIA WA BENKI**
**KWA MAELEKEZO YA BODI YA WAKURUGENZI**
**JUNI, 2025**



CamScanner